Fred Hutchinson Cancer Research Center
Chuo Kikuu cha Washington

# Fomu ya Ridhaa ya Muda ya Kushiriki katika Utafiti

Nambari ya Itifaki: ____________________

Jina la Mtafiti Mkuu: _______________________

*Kama wewe unahudumu kama mwakilishi aliyeamrishwa kisheria, mlezi, au unatoa ruhusa ya wazazi kwa mtoto katika utafiti huu, maneno "wewe" na "wako" yanarejelea mtu ambaye unatolea idhini au ruhusa ya kimzazi.*

## Unaulizwa kujiunga na utafiti

Unapaswa kuchukua muda wako wakati wa kuamua kama utajiunga na utafiti.
Unapaswa kujadili uamuzi huu na familia yako na marafiki.

Kabla ya kukubali kujiunga, tutakueleza:

1. Kwa nini utafiti unafanywa;
2. Ni nini kitakachofanyika wakati wa utafiti na taratibu zozote ambazo ni za jaribio;
3. Hatari na faida zinazotazamiwa ukijiunga na utafiti;
4. Njia nyingine za kujiunga na utafiti na hatari zake na faida;
5. Jinsi faragha na usiri wako utakavyolindwa;
6. Nani utakayewasiliana naye kwa maswali.

Wakati husika pia tutakueleza:

1. Nani anayelipia matibabu kama utajeruhiwa wakati wa utafiti;
2. Nafasi ya hatari ambayo hatuijui bado;
3. Kwa nini unaweza kuondolewa kwenye utafiti;
4. Gharama yoyote ya kushiriki katika utafiti;
5. Kitakachofanyika kama utaamua kuondoka kwenye utafiti;
6. Wakati utakapojifunza kuhusu matokeo mapya kuhusiana na utafiti;
7. Ni watu wangapi wamepangiwa utafiti;
8. Masomo yoyote ya hiari ambayo unaweza kushiriki.

Maelezo ya jaribio hili la kliniki ambalo litapatikana katika www.clinicaltrials.gov, kama inavyohitajika na Sheria za Marekani. Tovuti hii haitajumulisha maelezo ambayo yatakutambulisha. Kwa kiasi kikubwa, Tovuti itajumulisha muhtasari wa matokeo. Unaweza kutafuta kwenye Tovuti hii wakati wowote.

Fred Hutchinson Cancer Research Center
Chuo Kikuu cha Washington

# Fomu ya Ridhaa ya Muda ya Kushiriki katika Utafiti

## Haki zako

Sio lazima ujiunge na utafiti huu. Uko huru kusema ndio au la. Ikiwa utajiunga na utafiti huu, sio lazima ukae kwa utafiti. Unaweza kuacha wakati wowote (hata kabla ya kuanza). Hakuna adhabu kwa kusema la au kuacha. Huduma yako ya afya ya mara kwa mara haitabadilika.

Ikiwa utakuwa mgonjwa au utaumia katika utafiti, hautapoteza haki yoyote ya kisheria kutafuta malipo kwa kutia saini fomu hii.

Ikiwa utakubali kujiunga, utapata nakala ya fomu hii na nakala ya fomu ya ridhaa katika lugha ya Kiingereza ya utafiti wenyewe.

## Kwa maelezo zaidi

Unaweza kuwasiliana na mtafiti mkuu ________________ katika ________________ wakati wowote una maswali kuhusu utafiti au majeraha yanayohusiana na utafiti.

Unaweza pia kuwasiliana na Karen Hansen, Mkurugenzi wa Institutional Review Office, Fred Hutchinson Cancer Research Center katika 206-667-4867 kama una maswali kuhusu haki zako kama mshiriki au jambo la kufanya ikiwa utajeruhiwa.

## Saini

Ikiwa utaweka fomu hii sahihi, inamaanisha kuwa tumekuelezea utafiti, na umekubali kushiriki kwa hiari yako.

____________________________________________ ________________
Jina la Mshiriki Lililochapishwa na Saini au Mwakilishi Aliyeidhinishwa Kisheria, kama inahusika — Tarehe

____________________________________________________________
Uhusiano wa Mwakilishi Aliyeidhinishwa Kisheria kwa Mshiriki, kama inahusika

____________________________________________ ________________
Jina Lililochapishwa la Mkalimani/Shahidi na Saini — Tarehe